**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. JUMANNE ABDALLAH SAGINI (MB.) NA NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA PILI WA BARAZA LA PILI LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 ILIYOTOLEWA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA NSSF, MKOANI MOROGORO APRILI 19, 2024.**

**Dkt. Boniphace Luhende, Mwenyekiti wa Baraza, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Mark Mulwambo, Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Alice Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Mteule; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Zuhura Kussaga, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Stanley Mahenge, Naibu Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bw. Mtani Songorwa, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Bi. Sarah Rwezaula, Katibu wa TUGHE Ngazi ya Mkoa Dar es Salaam;**

**Bw. Nsubisi Mwasandenge, Mwakili wa TUGHE Taifa;**

**Viongozi wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana,**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**SOLIDARIIIIIITY;**

**MSHIKAMANOOO.**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuamsha salama na kutupa nafasi ya kukutana nanyi leo hii. Pili, napenda kuwashukuru kwa kunialika ili nifungue kikao hiki. Nitumie fursa hii kuipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kwa kuwa na Baraza la Wafanyakazi kwani zipo ofisi nyingi sana ambazo zimeshindwa kutekeleza takwa hili la kisheria.

Kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe kutoka TUGHE Mkoa wa Dar es Salaam, kwa kufanya kazi kwa karibu na Tawi la TUGHE la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha Baraza hili la Wafanyakazi

linafanya kazi kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria na kwa mujibu wa Mkataba kama alivyoeleza Mwenyekiti wa Baraza.

**Ndugu wajumbe wa Baraza;**

Nami niungane na Mwenyekiti kwa kuendelea kumshukuru Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo amekuwa akiiangalia Ofisi na kuiwezesha kwa kutoa nafasi mbalimbali za viongozi ndani ya Ofisi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba tangu kuanzishwa kwa Ofisi hii, imetoa viongozi wengi ikiwa ni pamoja na Majaji wa Mahakama Kuu, Wakuu wa Taasisi mbalimbali, Naibu Katibu Mkuu katika Wizara, wakurugenzi kwenye idara mbalimbali za sheria na kuinua baadhi ya viongozi kutoka ndani ya Taasisi kama alivyofanya kwa **Bi. Alice Edward Mtulo.** Uteuzi wako **Bi. Mtulo** ni ishara tosha ya namna ambayo Mhe. Rais alivyo na imani kubwa na Ofisi hii. Hivyo, ni matumaini yangu kwamba utatekeleza majukumu yako kwa juhudi na ufanisi mkubwa ili tuendelea kumsaidia Mhe. Rais katika ujenzi wa Taifa na shughuli za maendeleo.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Kwa nafasi nyingine tena nakupongeza sana Mwenyekiti kwa kuendelea kushirikiana na kutekeleza matakwa ya kisheria kwa kuhakikisha Baraza hili linafanyika tena mara ya pili kwa Mwaka wa fedha huu. Pia nakupongeza Bw. Mark Mulwambo kwa kutekeleza majukumu yako kama Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti kabla ya uteuzi wa Bi. Alice Mtulo. Nakupongeza sana kwa ushirikiano wako.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Baraza hili ni jukwaa muhimu sana mahala pa kazi kwani ni kiunganishi kati ya Menejimenti na Wafanyakazi. Ni matumaini yangu kuwa mtaendelea kushirikiana ili kuleta ufanisi kwa Mamlaka na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo niwakumbushe kuwa Serikali inazingatia sana suala la taasisi zake kuwa na Mabaraza ya Wafanyakazi kwani yalianzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri Serikali katika ngazi za Idara, Taasisi na Wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimali watu, utekelezaji wa majukumu, kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi, kutoa ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, maslahi ya watumishi na kusimamia haki na ustawi katika sehemu za kazi.

Aidha, ni wajibu wa mabaraza haya kuwa vyombo vya ushauri na usimamizi katika kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, pia wanazingatia maadili ya utumishi wao ili kuleta matokeo ya utendaji wa kazi yenye tija.

**Ndugu wajumbe wa Baraza;**

Kama tulivyosikia matunda ya kuwa na Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi yameanza kuonekana ndani ya OWMS. Matunda hayo ni pamoja na kuwashirikisha wafanyakazi katika maamuzi mbalimbali ikiwemo kuwasilisha changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi, kama ambavyo ilivyo sasa moja kati ya madhumuni ya mkutano huu ni kuwawezesha wafanyakazi kupitia makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa **2024/2025** kwa kuzingatia ukomo wa Bajeti, malengo ya Taasisi na maeneo ya vipaumbele.

Utaratibu huu unalenga kukuza uwazi na ushirikishwaji katika maamuzi mbalimbali ya Mamlaka ili mtumishi anapotekeleza majukumu yake awe akifahamu Dira na Dhima ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali zinamtaka afanye nini. Vilevile, mtumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali anapaswa kufahamu bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli zake ndani ya Taasisi ili afanye kazi kwa kuzingatia malengo na rasilimali zilizokadiriwa kutumika.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Nipende kuwakumbusha kwamba Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** imedhamiria kwa dhati kuondoa uzembe na vitendo vyote vya rushwa mahala pa kazi. Hii ni pamoja na kubana matumizi yasiyo ya lazima ili kuongeza tija. Hivyo, ni wajibu wa kila mtumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu Serikali kuhakikisha anafahamu wajibu wake mahali pa kazi, ili aweze kutekeleza majukumu aliyopangiwa na kuhakikisha anayakamilisha katika muda uliopangwa, hali kadhalika ahakikishe anatunza mali na vifaa alivyokabidhiwa kufanyia kazi. Bila kusahau wajibu wa kuwahi kazini, kufanya kazi kwa bidii na kuwa na uzalendo kwa taifa wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Kama tulivyofahamishwa kuwa Ajenda kuu ya Baraza hili ni kupokea na kujadili taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha **2024/2025** ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Ambapo nimeelezwa kwamba Ukomo

wa bajeti umeongezeka kutoka kiasi cha **Shilingi bilioni kumi na saba, milioni sabini na tano, laki nane na elfu hamsini (Tshs 17,075,850,000/=)** zilizotengwa Mwaka wa Fedha **2023/2024** hadi kufikia ukomo wa kiasi cha **Shilingi Bilioni ishirini, milioni mia saba hamsini, laki saba na elfu ishirini (Tshs. 20,750,720,000/=)** kwa Mwaka wa Fedha **2024/2025.** Ongezeko hilo ni **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni mia sita sabini na nne, laki nane na elfu sabini (Tshs. 3,674,870,000)** sawa na ongezeko la asilimia **21.52** ikilinganishwa na Bajeti inayoendelea ya Mwaka **2023/2024.** Ongezeko hilo la Bajeti litajikita katika kuongeza uwezo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kwenye malengo, vipaumbele, mipango na mikakati iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka ujao wa fedha.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Nitumie fursa hii kuishukuru Serikali ya awamu ya sita (06) inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi inavyoiwezesha Ofisi hii. Ongezeko la bajeti ni ishara kubwa kwamba Mhe. Rais anatambua mchango mkubwa wa Ofisi hii katika kuiwakilisha Serikali na Taasisi zake katika mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Jitihada zenu za kuendelea kuokoa fedha ambazo zingelipwa kama tungeshindwa kwenye mashauri mbalimbali kama ilivyoelezwa ni mchango mkubwa katika kuisaidia Serikali kupeleka fedha katika shughuli za maendeleo.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Nimefurahishwa sana kusikia taarifa yenu ya mafanikio mbalimbali mliyopata katika kutekeleza majukumu yenu. Haswa haswa ushindi wenu katika mashauri yanayohusisha mabilioni ya fedha za watanzania ikiwamo shauri la Usuluhishi baina ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja (PBPA) na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Kampuni ya Alchemist Energy Traiding DMCC kutoka Umoja wa Falme za Kiarabu ulioipa serikali ushindi wa zaidi ya **Dola za Marekani 14,457,182.33** (Takriban bilioni 36.9 za fedha za kitanzania)

Pia mashauri yenye maslahi mapana kwa taifa ikiwamo shauri la bomba la mafuta *(Center for Food and Adequate Living Rights and 3 Others Versus Attorney General of UG and Others, Reference No. 39/2020)*, mashauri yaliyohusisha mkataba wa Bandari *(Alphonce Lusako & 3 Others vs. The Attorney General & 3 Others, Misc. Civil Cause No. 5 of 2023; Meczedeck Maganya v. The Attorney General & 2 Others, Misc. Civil Cause No 9 of 2023; and Fredrick Attorney Mboma Vs AG), na shauri* la Kiwanda cha Chalinze Cement (Fair Competition Tribunal Versus Scancem International DA, Tribunal Application No. 16/2023) na mashauri mengi aliyoeleza mwenyekiti. Hongereni sana kwa kazi nzuri.

Ushindi huu unaonesha wazi kuwa Ofisi hii inawajibika vyema katika kutekeleza majukumu yake. Pia unaonesha wazi kuwa Sekta ya sheria nchini iko imara na tayari kutatua matatizo ya wananchi, wafanyabiashara na wawekezaji. Tunaimani ubora mnaoonoesha kwenye kuendesha mashauri haya kutakuwa kivutio kikubwa kwa

wawekezaji nchini  ambao watajione wenye uimara wa sekta yetu ya sheria katika kila Nyanja.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Nimeona wazi kuwa idadi kubwa ya mashauri mnayoshughulikia ni mashauri ya ardhi. Pia nimefurahi kusikia mikakati mliyojiwekea katika kutatua mashauri hayo. Ninaahidi Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kushirikiana na Wizara ya Ardhi ili kuendelea na jitihada za kupunguza migogoro ya ardhi kwa kuweka mikakati bayana ya kushughulikia migogoro hiyo kabla ya kuwasilisha mahakamani au kwenye mabaraza ya ardhi. Ni Imani kuwa kushughulikia kwa mashauri haya mapema iwezekanavyo kutapunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya mashauri ya ardhi.

Pia Wizara itaendelea kufanya mawasiliano na taasisi mbalimbali za Serikali ili kuweza kutoa elimu kuhusu usimamizi bora wa mikataba, pamoja na ushauri juu ya hatua mbalimbali za kuchukua ili kuepuka kuwa na migogoro isiyo na lazima.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Sanjali na hayo, Wizara kama chombo chenye mamlaka ya kuisimamia Taasisi zote za sheria na kuhakikisha kuwa utendaji wake uko sambamba na malengo yaliyowekwa na Serikali, itapenda mara kwa mara kupatiwa taarifa za utekelezaji za robo mwaka, nusu mwaka, na za mwisho wa mwaka, ambazo zitabainisha taarifa za mapato na matumizi ya fedha, taarifa za uendeshaji wa Mashauri ndani na nje ya nchi, taarifa

kuhusu rasilimali watu na pia jinsi gani umakini katika uendeshaji wa mashauri unazingatiwa.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza**

Kama Wizara naomba kuwahakikishia kuwa tutaendelea kuwaunga mkono kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya licha ya changamoto ambazo zimekuwa zikiwakabili na ninaahidi kwamba changamoto ambazo mmenieleza nimezichukua na tutazishughulikia kwa kushirikiana na viongozi wenzangu ikiwa ni pamoja na kuziwasilisha zile changamoto za kiutumishi ili ziweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za Utumishi wa Umma.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Naomba kuwasihi kuendelea kujiepusha na migongano isiyo na tija hasa migogoro na migongano kati ya Menejimenti, Watumishi na Chama cha Wafanyakazi (TUGHE), kwa kuwa kuendeleza migogoro husababisha ufanisi wa kazi kushukuka au kutoonekana na hivyo kuifanya Wizara ishindwe kutimiza azma yake ya kuisimamia vizuri Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

**Ndugu Wajumbe wa Baraza;**

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwasihi mtumie muda wenu vizuri katika kujadili hoja mbalimbali katika kikao hiki kwa ufanisi mzuri. Ni matumaini yangu mtalitumia baraza hili kuhimiza kila mtumishi ajue wajibu wake wa kutumia muda wa kazi ipasavyo kwa kufanya kazi kwa

bidii ili kuiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kusonga mbele katika kutekeleza maagizo ya serikali pamoja na kutoa huduma kwa wakati.

Baada ya kusema haya, sasa natamka rasmi kuwa Mkutano wa pili wa Baraza la Pili la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serkali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, umefunguliwa rasmi.

**AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA**.